

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII



TARATIBU ZA UINGIZAJI BIDHAA KUTOKA NJE YA NCHI

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi iliyoko chini ya Wizara ya Afya inayodhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba nchini. Mamlaka ya Chakula na Dawa imeweka taratibu za kufuata wakati wa kuingiza chakula, dawa, vipodozi au vifaa tiba ili kuzuia bidhaa duni, zisizo salama na bidhaa bandia kuingizwa nchini. Hioi hufanyika kwa lengo la kulinda afya za walaji.

Taratibu hizi pia husaidia kuhakikisha bidhaa zenye lebo na maelezo sahihi tu ndizo zinazolingia nchini. taratibu hizi husaidia kuwalinda wafanyabiashara waaminifu dhidi ya ushindani wa bidhaa zisizo na viwango nyenye ubora unaokubalika.

Wale wote wenye nia ya kuingiza bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA, ni lazima wasajiliwe na Mamlaka. Aidha bidhaa inayokusudiwa kuingizwa nchini, lazima iwe imesajiliwa na TFDA.

Waingizaji waqliokwishasajiliwa na TFDA wanalazimika kuomba kibali cha Mamlaka kila wanapotaka kuingiza bidhaa nchini.

Wakati wa kuomba kibali, muagizaji atawajibika kujaza fomu maalumu ya maombi ikiambatana na Ankara kifani (Profoma Invoice) kutoka kwa mtengenezaji, yenye taarifa zote zinazohusisna na bidhaa zinazotarajiwa kuagizwa. Taarifa hizo ni kama vile:

- Jina kamili la bidhaa (Generic and Brand name)
- Jina la mtengenezaji
- Namba ya usajili wa bidhaa
- Muda wa mwisho wa matumizi ya bidhaa
- Kiasi cha bidhaa kinachoagizwa
- Nchi bidhaa inakotoka
- Mpaka utakaotumika kuingiza mzingo/bidhaa nchini
- Thamani ya mzingo
- Njia za usafirishaji
-

Ankara kifani hii itaambatana na fomu maalumu ya maombi na zitatumwa kwa Mkurugenzi Mkuu, TFDA.

Baada ya kuyapitia maombi haya ya vibali, ruhusa ya kuingiza bidhaa hutolewa. Kibali hiki ni kwa ajili ya mzigo wa bidhaa ulioombewa ruhusa tu, na inweza kutumika ndani ya kipindi cha miezi (6) sita, tangu kilipotolewa kwa mzigo husika. Baada ya kipindi hiki, kama mzigo wa bidhaa utakuwa haujaingia nchini, kibali huisha muda wake na maombi mengine ni lazima yafanyike.

Mzigo wa bidhaa husika unapofika mpakani, hukaguliwa na wakaguzi wa TFDA ili kuthibitisha kuwa ndio mzigo ulioombewa kibali. Pia taarifa zote zilizoandikwa kwenye Ankara kifani hupiiwa kwa uthibitisho.

Mkaguzi huweza kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara pale anapohisi kuna tatizo. Kwa dawa za kutibu malaria, viuvavijisumu (antibiotics) na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, ni lazima uchunguzi wa kimaabara ufanyike mpakani kabla hazijaingia nchini.

Dawa hizi ni lazima kufanyiwa uchunguzi ili kuhakiki ubora wake. Mkaguzi akiridhika huweka muhuri na mzigo huruhusiwa kuingia nchini.

Bidhaa ambazo ubora wake utakuwa wa mashaka, huzuiwa kuingia na sampuli kutumwa maabara kubwa ya TFDA kwa uthibitisho zaidi. Zile bidhaa ambazo hazitafikia kiwango, hazitaruhusiwa kuingizwa nchini bali zitarudishwa zilikotoka au kuteketezwa kwa gharama ya muagizaji.

TFDA inawaomba waagizaji wa bidhaa kutoa ushirikiano ili kuhakikisha taratibu zinafuatwa na wananchi wanapata bidhaa boora na salama.

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)
S. L. P 77150
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2450512/2450751/2452108
Fax: 255 22 2450793
Email: tfda@simbanet.net
Tovuti: www.tfda.or.tz